

KUSHUKA KWA HADHI YA LUGHA ZA JAMII NCHINI TANZANIA

YOHANA P. MSANJILA

University of Dar es Salaam, Tanzania

ABSTRACT

Lugha za jamii hapa nchini kama zilivyo lugha nyingine barani Afrika zinakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka lugha zilizoendelea ambazo hutumika rasmi kitaifa na kimataifa. Kabla ya Tanganyika (sasa Tanzania) kupata uhuru wake (1961), lugha za jamii zilikuwa na hadhi ya juu kijamii kuliko ilivyo sasa. Hii ilitokana na lugha hizo kutumika katika utawala wa ngazi za chini. Huku kushuka hadhi kwa lugha za jamii kumetokana na mabadiliko ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mabadiliko haya yalisisitiza umuhimu wa sera ya lugha kukuza na kuendeleza lugha moja muhimu ili kujenga umoja wa kitaifa. Ili kuinua hadhi ya lugha za jamii hapa nchini, makala haya yanapendekeza zitumike mbinu mbalimbali zifuatazo: Kwanza, wazungumzaji wa lugha hizi wahimizwe kutumia lugha zao za jamii mara kwa mara. Pili, sera ya lugha ya Tanzania ifanyiwe marekebisho ili itoe nafasi kwa lugha za jamii kutumika rasmi. Tatu, vyombo vya habari navyo vihimizwe kutumia lugha za jamii katika mawasiliano yake na nne, lugha za jamii zipewe haki ya kutumika kisheria hapa nchini.

Keywords: Kushuka Hadhi Lugha za Jamii

1. UTANGULIZI

Tanzania ina lugha za jamii zaidi ya 120 (Whiteley 1969; Batibo 1992) na Kiswahili ni miongoni mwa lugha hizo. Tunatumia lugha za jamii kwa maana ya lugha za makabila, lugha za asili, lugha za kienyeji, lugha ndogondogo au lugha za kimbari. Abdulaziz-Mkilifi (1972) amezigawa lugha za Tanzania katika makundi makuu matatu yafuatayo: *lugha za jamii*, *Kiswahili* na *Kiingereza*. Mgao huu wa Abdulaziz-Mkilifi umezingatia zaidi hadhi kuliko uamilifu wa lugha zenyewe. Kijamii, Kiingereza kinapewa hadhi ya juu zaidi kuliko Kiswahili na lugha za jamii. Kiingereza, ni lugha ya Kimataifa inayotumika katika nyanja zote za mawasiliano ya kijamii, kiuchumi, katika sayansi na tekinolojia ya kisasa, katika utawala na siasa, katika elimu na mahakama za juu, katika mawasiliano ya kimataifa na kidiplomasia.

Kwa upande mwingine, Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania, Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Pia Kiswahili kinatumika kwa kiasi fulani katika nchi za Burundi, Rwanda, Malawi, Zambia, Zimbabwe na katika visiwa vya Comoro. Nchini Tanzania, Kiswahili kinatumika serikalini, shuleni, jeshini, bungeni, mahakama za mwanzo, na katika siasa. Ni lugha inayowaunganisha watu wa makabila mbalimbali nchini Tanzania. Lugha za

jamii, zinatumiwa zaidi vijijini ambako ndiko wazungumzaji wake wengi waliko. Lugha hizi zinatumiwa zaidi katika maeneo yasiyo rasmi kama vile nyumbani, sehemu za starehe, kwenye matambiko n.k. Lugha za jamii hazitumiwa kabisa shuleni.

Tafiti mbalimbali zilizofanywa na wanazuoni juu ya lugha za jamii nchini Tanzania, zinaonyesha kwamba lugha za jamii ziko hatarini kutoweka ikiwa juhudi za makusudi hazitachukuliwa kuzinusuru (Batibo 1992; Mekacha 1993; Heine 1992; Msanjila 1999). Matokeo ya tafiti hizo yanaonyesha kwamba mbali na idadi ya wazungumzaji wa lugha za jamii kupungua, vijana wengi wa umri wa kuanzia miaka 14 hadi 35 ambao ndio wadumishaji wakuu wa lugha, hutumia Kiswahili zaidi kuliko lugha za jamii. Hivyo basi, kwa kuzingatia maelezo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusiana na lugha za jamii, makala haya yanakusudia kuchunguza mambo matatu yafuatayo: kwanza, kujadili dhana ya hadhi ya lugha kwa ujumla ili kuwa msingi wa majadiliano yetu; Pili, kuchunguza sababu za msingi zinazofanya hadhi ya lugha za jamii kushuka; na tatu, kujadili namna ya kuinua hadhi ya lugha za jamii hapa nchini.

2. DHANA YA HADHI YA LUGHA KWA UJUMLA

Tunaposema lugha fulani ina hadhi ya juu, tuna maana kwamba lugha hiyo inamnufaisha mzungumzaji kijamii, kiuchumi, kielimu, kikazi na hata kisiasa (Heine 1992). Kwa kawaida, lugha yenye hadhi ya juu kijamii hutambuliwa na kutumiwa na tabaka tawala katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kimataifa. Lugha yenye hadhi ya juu kijamii humsaidia mzungumzaji siyo tu kupata kazi nzuri, kupata maisha bora zaidi, bali pia humsaidia mzungumzaji kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yake.

Lugha za Ulaya na hususani zile zilizokuwa zikitumiwa katika utawala wa kikoloni barani Afrika, bado hadi leo lugha hizi zinapewa hadhi ya juu kijamii kuliko lugha za jamii. Lugha kama Kiingereza, Kifaransa, Kireno n.k. bado zinapewa hadhi ya juu katika nchi zilizowahi kutawaliwa na wakoloni kutokana na lugha hizo kuhusishwa na maendeleo ya kiuchumi na matumizi ya sayansi na tekinolojia ya kisasa. Kwa maneno mengine na ambacho hakisemwi hapa ni kwamba lugha za jamii zinapewa hadhi ya chini si kwa sababu nyingine bali ni kwa sababu lugha hizi hazihusishwi na maendeleo ya juu ya kiuchumi. Lugha kuhusishwa na maendeleo ya kiuchumi tuna maana kwamba lugha hizo zinatumiwa kama lugha muhimu za mawasiliano katika kuelezea maendeleo ya sayansi na tekinolojia ya jamii hizo.

Tunapenda ieleweke hapa kwamba suala la hadhi ya lugha kuhusishwa na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa na nchi zilizoendelea linapaswa kuangaliwa upya na kwa makini zaidi. Tunasema hivi kwa sababu hadhi ya lugha hupimwa kwa kuzingatia uamilifu wa lugha zenyewe katika kukidhi mahitaji na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa na jamii hizo. Wakati lugha za jamii zinatoshleza kuelezea utamaduni na maendeleo ya kiuchumi ya Mwafrika

kwa ufasaha, lugha za Ulaya zinapwaya kuelezea kwa ukamilifu utamaduni na maendeleo ya kiuchumi ya Mwafrika.

Mjadala wa hapo juu unatufanya tujiulize swali, kwa nini katika mazingira ya Kiafrika lugha za jamii zionekane kuwa na hadhi ya chini wakati lugha hizo zina uwezo wa kuelezea kwa ufasaha maendeleo ya kiuchumi ya Afrika? Kwa maneno mengine, kwa nini hadhi ya lugha za jamii zisihusishwe na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa miongoni mwa jamii za Kiafrika zenyewe? Kwa maoni yetu, tunafikiri kwamba tatizo hapa linatokana na uelewa wa dhana ya hadhi ya lugha. Inaelekea kwamba baadhi ya wanazuoni (Abdulaziz-Mkilifi 1972; Brauner et al. 1978; Blommaert 1990) wamekuwa wakielezea hadhi ya lugha za jamii kwa mtanzamo uliozoeleka wa kuhusisha na maendeleo ya juu ya kiuchumi yaliyofikiwa na jamii zilizoendelea.

Kwa maoni yetu, lugha za jamii barani Afrika au katika nchi zinazoendelea hazipaswi kupimwa hadhi zake kijamii kwa kuhusishwa na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa katika nchi zilizoendelea. Hali kadhalika, siyo haki kupima hadhi ya lugha za Ulaya kwa kuhusisha na maendeleo ya kiuchumi yaliyofikiwa na nchi za Kiafrika au nchi zinazoendelea. Kimsingi hapa, suala la hadhi ya lugha linafaa liangaliwe kwa makini na ikiwezekana lizingatie dhima za lugha zenyewe katika kukidhi mahitaji na maendeleo ya kiuchumi ya jamii zinazohusika. Sehemu inayofuata tutachunguza hali halisi ya hadhi ya lugha za jamii nchini Tanzania hususani vijijini.

2.1 KUSHUKA KWA HADHI YA LUGHA ZA JAMII

Katika utangulizi wetu tumesema kwamba lugha za jamii nchini Tanzania zina hadhi ya chini kabisa ukilinganisha na Kiingereza na Kiswahili. Pia katika sehemu ya 2. hapo juu tumesisitiza kwamba hadhi ya lugha isipimwe kwa kuhusisha tu na maendeleo ya juu ya kiuchumi yaliyofikiwa na jamii zilizoendelea bali pia izingatie uwezo wa lugha hiyo katika kukidhi mahitaji na maendeleo ya jamii husika. Kwa kuzingatia maelezo haya, sasa tunashawishika kuchunguza sababu zinazofanya lugha za jamii ziwe na hadhi ya chini. Zipo sababu nyingi, lakini kwa mujibu wa makala haya tutajadili sababu kuu mbili. Kwanza, lugha za jamii hazitumiki katika mawasiliano rasmi ya jamii na pili, ni udhaifu wa Sera ya Lugha. Tuanze na sababu ya kwanza.

2.1.1 Lugha za Jamii Hazitumiki katika Mawasiliano Rasmi

Lugha yoyote hupewa hadhi ya juu kijamii ikiwa lugha hiyo inatambuliwa na kutumika katika shughuli za kiserikali. Kimantiki, ni kwamba lugha yoyote isiyotumika katika shughuli rasmi za kiserikali, hadhi ya lugha hiyo hushuka. Kabla ya kufikia karne ya 5, lugha ya Kilatini ilikuwa na hadhi ya juu kijamii kuliko Kiingereza kwa sababu Kilatini kilikuwa kikitumika kama lugha rasmi ya dola kwa wakati huo (Milroy, 1984). Kilatini kilitumika katika elimu ya juu,

mahakama za juu, katika biashara za kimataifa, na katika taaluma mbalimbali. Kwa kawaida, lugha za hadhi ya juu huwa zina sifa teule ambazo huwa hazipatikani kwa wingi katika lugha zenye hadhi ya chini yaani lugha za jamii.

Heine (1992) anazitofautisha lugha za hadhi ya juu kijamii na zile za hadhi ya chini kwa kutaja sifa teule zifuatazo:

Lugha za Hadhi ya Juu	Lugha za Hadhi ya Chini
- zimesanifiwa na zinatumiwa lugha rasmi	- hazikusanifiwa na zinatumiwa lugha isiyo rasmi yaani ya kilahaja au kikanda
- nyingi ya lugha hizi zinatoka Ulaya au nchi zilizoendelea kiuchumi	- nyingi ya lugha hizi ni lugha za makabila ya ndani ya nchi
- zinatumiwa kama lugha za kufundishia katika mfumo rasmi wa elimu. Baadhi ya wazungumzaji hujifunza lugha hizi shuleni kama lugha yao ya pili.	- hutumiwa kama lugha ya kutolea elimu katika mfumo usio rasmi. Wazungumzaji hujifunza lugha hizi nyumbani au kwa wanajamii wenyewe
- zinakuzwa na kuenezwa kwa kuwa na mipango madhubuti iliyoandaliwa katika sera ya lugha. Maeneo ya matumizi ya lugha hizi huainishwa katika sera ya lugha na ni rahisi kwa mzungumzaji kupata kazi nzuri kwa kutumiwa lugha hizi.	- hakuna mpango madhubuti ulioandaliwa katika sera ya lugha ili kuzikua na kuzieneza lugha hizi. Hazitumiwa katika mazingira rasmi ya kazi
- zina historia ndefu ya karne nyingi zilizopita ya kuwa na maandishi yaliyohifadhiwa ya lugha hizi	- zina historia ya karne nyingi zilizopita ya kupokezana kwa njia ya mdomo au kurithishana lakini si kwa njia ya maandishi.
- lugha hizi pia hutumiwa na watu wenye nafasi za juu serikalini, katika siasa, uchumi, elimu, dini nk.	- lugha hizi hutumiwa na watu wa kawaida ambao wengi wao huishi vijijini.

Kwa mujibu wa sifa hizi teule zilizotolewa na Heine (1992) tunaweza kusema kwamba lugha za jamii nchini Tanzania ziko katika kundi la lugha zenye hadhi ya chini. Tunaziweka lugha za jamii katika kundi hili siyo kwa sababu hazina uwezo wa kuwa na sifa teule za lugha zenye hadhi ya juu, la hasha, ukweli ni kwamba lugha za jamii hazipewi kipaumbele cha kukuzwa na kuendelezwa na serikali kama ilivyo kwa lugha ya Kiswahili. Ikumbukwe kwamba kabla ya Tanganyika kupata uhuru wake mwaka 1961, lugha za jamii zilikuwa na hadhi ya kuridhisha na kukubalika kijamii. Hii ilitokana na ukweli kwamba mfumo wa utawala wa kikoloni wa wakati huo uliruhusu lugha za jamii kutumiwa katika mawasiliano ya utawala wa chini ili kuwafikia watu wa makabila yote. Lugha za jamii zilitumiwa katika mikutano ya hadhara, mabaraza ya usuluhishi, kanisani,

katika elimu ya watu wazima nk. Kiswahili kilitumika kama lugha ya mawasiliano na watawala wa ngazi ya kati yaani, wilayani na mikoani (zamani majimbo). Aidha, lugha ya Kiingereza ilitumika kuwasiliana na watawala wa ngazi ya juu kitaifa. Kwa kuwa lugha za jamii ziliruhusiwa kutumika katika utawala wa ngazi za chini za vijiji, lugha za jamii nyingi zilifanyiwa utafiti na Wamisionari hadi kufikia lugha hizo kuandikiwa vitabu. Baadhi ya vitabu hivyo ni biblia, katekesimo, vitabu vya nyimbo, sarufi za lugha mbalimbali, hadithi na vitabu rahisi vya kujifunza kusoma na kuandika.

Baada ya uhuru, mambo yalibadilika. Lugha za jamii zilinyimwa uhuru wa kutumika katika utawala wa serikali za vijiji. Ilidaiwa kwamba kuendelea kutumia lugha za jamii katika utawala wa vijiji kungesaidia kujenga ukabila na kuhatarisha umoja wa kitaifa. Kutokana na sababu hii, Kiswahili kilipewa msukumo wa kukuzwa na kuendelezwa na serikali yenyewe. Kimsingi, hadhi iliyonayo Kiswahili kijamii imetokana na mipango ya makusudi ya serikali iliyoandaa kupitia sera yake ya lugha na kutekelezwa na vyombo vilivyopewa jukumu hilo ili Kiswahili kiweze kukidhi mahitaji ya jamii ya sayansi na tekinolojia.

Lugha za jamii zina hadhi ya chini si kwa sababu nyingine bali wazungumzaji wake hawazitumii kikamilifu katika kuelezea mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi yanayotokea katika jamii. Wakati mfumo wa maisha ya jamii umebadilika kutoka uchumi wa kutegemea kilimo cha jembe la mkono peke yake na kuingia katika uchumi ulioendelea wa soko huria, hakuna mipango yoyote iliyofanywa na serikali ya kuzikuza na kuziendeleza lugha hizi za jamii ili ziweze kukidhi mahitaji ya mabadiliko haya ya maendeleo ya kiuchumi. Huko vijijini ambako lugha za jamii zinatumiwa kwa wingi, bado Kiswahili kinatumika zaidi kuliko lugha za jamii katika maeneo muhimu kama ya: shuleni, hospitalini, mahakamani (mahakama za mwanzo), kanisani, msikitini na maeneo mbalimbali ya biashara. Tunapenda kuisisitiza hapa kwamba ikiwa hatua za makusudi hazitachukuliwa kuziendeleza lugha hizi, hadhi ya lugha za jamii nchini Tanzania zitaendelea kushuka chini zaidi kwa sababu zitashindwa kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kisasa ya jamii.

2.1.2 Udhaifu wa Sera ya Lugha

Katika utangulizi wetu (1.) tumesema kwamba sera ya lugha inaweza kuhatarisha uhai wa lugha za jamii lakini hoja hii hatukuijadili zaidi. Sasa umefika wakati muafaka wa kuijadili. Kimsingi, sera ya lugha huandaliwa na Wizara maalumu iliyopewa jukumu hilo. Sera ya Utamaduni ya Tanzania (1997) ambayo huelezea sera ya lugha, imeandaliwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Sera ya lugha ni mwongozo wa kiutekelezaji unaohakikisha kwamba lugha zilizomo katika nchi husika, zinatumiwa sawasawa kulingana na mipango ya nchi hiyo. Robert Kaplan na Richard Baldauf (1997) na Mekacha (2000: 126) wote wanaelezea madhumuni ya sera ya lugha kuwa yanahusu:

Kushuka kwa Hadhi ya Lugha za Jamii Nchini Tanzania

- (i) *Kulinda uasili wa lugha usichafuliwe kutokana na mwingiliano wa kimsamiati kutoka lugha nyingine (kama wanavyofanya Wafaransa kulinda Kifaransa kisiharibiwe).*
- (ii) *Kufanyia lugha mabadiliko ili kuiondolea sifa za ubaguzi wa kijinsia (kama inavyofanywa kuhusiana na lugha ya Kiitaliano huko Italia).*
- (iii) *Kuhuisha (ua kufufua) matumizi ya lugha iliyotoweka ili iweze kutumika tena kama ilivyofanywa kuhusiana na lugha ya Kiebrania nchini Israel.*
- (iv) *Kurekebisha lugha ili iweze kutumika katika maeneo rasmi (kama ilivyofanywa kwa lugha ya Kituruki nchini Uturuki).*
- (v) *Kuteua na kusanifisha lugha ili iweze kutumika katika maeneo rasmi (kama ilivyofanywa kwa Kiswahili Afrika Mashariki).*
- (vi) *Kueneza matumizi ya lugha katika maeneo na jamii ambamo ilikuwa haitumiki awali.*
- (vii) *Kulinda lugha ambayo matumizi yake yako hatarini kutoweka.*
- (viii) *Kupanua mfumo, kuendeleza msamiati na kusawazisha mitindo ya lugha.*

Kwa kuzingatia madhumuni yaliyotajwa hapo juu, tunaweza kuyajumuisha madhumuni hayo katika makundi makuu matatu yafuatayo: *Kukuza, kueneza na kudumisha au kuhuisha lugha*. Wakati sera ya lugha ya Tanzania inatamka kwamba Kiswahili kitakuzwa, kitaenezwa na kuimarishwa, sera hiyo haisemi chochote kuhusu kuzikuza, kuzieneza au kuziimarisha lugha za jamii. Pamoja na ukweli kwamba sera ya lugha inathamini umuhimu wa lugha za jamii kwa kutamka kuwa ni hazina kuu ya historia, mila, desturi, tekinolojia, utamaduni na ni msingi wa lugha ya taifa (Sera ya Utamaduni 1997: 17), bado haitamki wazi ni jinsi gani lugha hizi zitakuzwa, zitaenezwa au kuimarishwa. Chunguza matamko ya Sera ya Lugha ya Tanzania kuhusu lugha za jamii katika mifano ifuatayo:

- (a) *Jamii zetu zitaendelea kutumia na kujivunia lugha zake za asili.*
- (b) *Wananchi, mashirika ya umma na ya watu binafsi yatahamasishwa kuandika, kukusanya, kutafiti, kuhifadhi na kutafsiri lugha za asili katika lugha nyinginezo.*
- (c) *Uandishi wa kamusi na vitabu vya sarufi za lugha za asili utahimizwa.*
- (d) *Mashirika ya umma na ya watu binafsi, yatahimizwa kuchapisha na kusambaza maandiko katika lugha za asili (Sera ya Utamaduni 1997: 17–18).*

Tamko la (a) hapo juu linaeleza kuwa lugha za jamii zitaendelea kutumika na jamii zinazohusika na lugha hizo. Sera ya lugha haisemi chochote kuhusu lugha za jamii kutumika nje ya mipaka ya jamii za lugha hizo. Pia Sera ya lugha haisemi chochote kuhusu kuziimarisha lugha hizi ili ziweze kutumika katika mawasiliano rasmi. Mkazo wa lugha hizi umewekwa katika kujivunia lugha hizo na siyo katika kuzikuza au kuzieneza. Ni ukweli usiopingika kwamba lugha

yoyote isipokuzwa au kutumika katika maeneo mengine mapya, hupoteza umaarufu wake na hadhi yake hushuka.

Kuhusu matamko (b), (c) na (d) hapo juu yanaonyesha kwamba kazi za kuandika, kutafiti, kuhifadhi na kuchapisha matokeo ya lugha za jamii zimeachwa mikononi mwa wananchi wenyewe na mashirika ya umma ya watu binafsi. Swali la kujiuliza hapa ni kwamba kwa nini majukumu yanayohusu lugha za jamii yaachwe kwa wananchi na mashirika ya umma ya watu binafsi na siyo kwa BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa) ambalo ndilo lenye jukumu la kukuza, kueneza na kuimarisha lugha? Kwa upande wa Kiswahili, sera ya lugha ya Tanzania imetamka wazi kwamba serikali itatoa msaada wa kukiimarisha Kiswahili ili kiweze kuendelea na kutumika. Chunguza matamko yafuatayo:

- (a) *Vitawekwa vivutio kwa watu binafsi na mashirika mbalimbali kuchapisha na kusambaza maandiko katika lugha ya Kiswahili.*
- (b) *Baraza la Kiswahili la Taifa litakuwa na jukumu la kutafiti, kuneemesha na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili.*
- (c) *Baraza la Kiswahili la Taifa na Taasisi nyingine za ukuzaji wa Kiswahili zitaimarishwa na kupatiwa nyenzo na fursa ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu (Sera ya Utamaduni 1997: 16–17).*

Matamko haya ya sera ya lugha yanaonyesha tofauti iliyopo kati ya Kiswahili na lugha za jamii. Kama tulivyosema huko nyuma katika 2.1.1. ni kwamba lugha za hadhi ya juu zinawezeshwa na serikali kufikia hapo zilipo, wakati lugha za jamii zinaachwa bila kusaidiwa. Kwa kuzingatia mfano wa lugha ya Kiswahili, serikali imeweka vivutio kwa watu binafsi na mashirika mbalimbali ili yafanye shughuli za utafiti zinazohusiana na Kiswahili. Hali kadhalika BAKITA limepewa jukumu la kutafiti, kuneemesha na kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika maeneo mapya. Ili kuhakikisha kwamba Kiswahili kinaendelea kutumika katika nyanja mbalimbali, serikali inatoa msaada (nyenzo) kwa BAKITA na Taasisi nyingine za ukuzaji wa Kiswahili ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Ikumbukwe hapa kwamba misaada inayotolewa na serikali ya kuisaidia lugha ya Kiswahili iendeleo na kuimarika, misaada kama hiyo (k.m. iliyotajwa katika (e), (f) na (g) hapo juu) siyo tu kwamba haitolewi kwa lugha za jamii bali pia haitamkwi katika sera ya lugha. Wakati lugha za jamii zimeachwa ziendelezwe na wananchi wenyewe, lugha ya Kiswahili inaendelezwa na serikali na imeundiwa vyombo (k.m. BAKITA, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, n.k.) vya kuhakikisha kwamba Kiswahili kinaendelezwa ili kitumike katika nyanja zote za mawasiliano ya kijamii. Huu ni ushahidi tosha wa kuthibitisha kwamba sera ya lugha ya Tanzania inadhoofisha kwa makusudi maendeleo ya lugha za jamii ili zisiweze kushindana na Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa. Je, lugha za jamii zitaendelea kupuuzwa hadi lini? Sehemu inayofuata inajadili mbinu mbalimbali zinazofaa kutumika ili kuinua hadhi ya lugha za jamii.

3. MBINU ZA KUINUA HADHI YA LUGHA ZA JAMII

Kabla ya kuanza majadiliano yetu, hebu tujiulize swali hili: je, lugha za jamii bado zina umuhimu wa kuendelea kutumika katika jamii zetu za sasa? Umuhimu wa lugha kutumika au kutotumika katika jamii hutegemea sana wazungumzaji wa lugha hizo. Wakizungumzia lugha ya Kifaransa iliyozungukwa na lugha ya Kiingereza katika jimbo la Quebec nchini Canada, Rene Appel na Pieter Muysken (1987) wanasema kwamba watetezi wakuu wa lugha ndogondogo mara nyingi huwa ni vijana waliokulia katika tamaduni za lugha hizo ambao huhakikisha kwamba maslahi ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya lugha hizo ndogondogo yanalindwa. Huku kulindwa na kutetewa kwa lugha ya Kifaransa katika jimbo la Quebec nchini Canada kunatokana na wazungumzaji wenyewe wa Kifaransa kuiona lugha yao kuwa bado ni ya muhimu katika mambo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Kwa upande wa Tanzania ni kwamba wazungumzaji wengi wa lugha za jamii waishio vijijini bado wanazithamini lugha zao za jamii na kuziona kuwa ni za muhimu siyo tu kwao bali pia kwa watoto wao (Mekacha 1993; Msanjila 1999). Ukweli ni kwamba lugha za jamii ni hazina kuu ya historia, mila, desturi, tekinolojia, utamaduni na ni msingi wa lugha ya taifa (Sera ya Utamaduni, 1997: 17). Mbali na sababu hizi, lugha za jamii ni kiungo muhimu cha ujenzi wa utamaduni wa Kiafrika (Kihore 1983). Hoja zote hizi zinadhihirisha kwamba lugha za jamii bado zina umuhimu wa kuendelea kutumika katika jamii zetu mbalimbali. Kwa maoni yetu tunafikiri kwamba ili lugha za jamii ziendeleo kutumika na watu wengi, tunahitaji kuinua hadhi ya lugha hizi kwa kutumia mbinu mchanganyiko zifuatazo: kuhimiza matumizi ya lugha za jamii, sera ya lugha kutazamwa upya, kuhimiza matumizi ya lugha za jamii katika vyombo vya habari na lugha za jamii kupewa haki ya kutumika kisheria. Hebu tuanze na mbinu ya kwanza.

3.1 KUHIMIZA WAZUNGUMZAJI KUTUMIA LUGHA ZA JAMII

Watumiaji wakuu wa lugha za jamii huko vijijini ni wazee, wanawake na watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu (Mekacha 1993; Msanjila 1999). Makundi mengine ya jamii kama: vijana, wasomi, wafanyakazi na wafanyabiashara hutumia zaidi Kiswahili kuliko lugha za jamii. Tunaposema kwamba tunataka kuhimiza wazungumzaji watumie lugha za jamii tuna maana ya kuwalenga hawa vijana, wasomi, wafanyakazi na wafanyabiashara waishio vijijini ili wajenge mazoea ya kutumia lugha za jamii mara kwa mara kama njia mojawapo ya kukuza na kuziendeleza lugha hizi. Hili linawezekana kwa sababu asilimia zaidi ya 99 ya wakazi wa vijijini ni watu wa asili na lugha moja (Msanjila 1999). Ikumbukwe hapa kwamba hata makundi haya yanayozungumza zaidi Kiswahili kuliko lugha za jamii ni makundi yanayotokana na jamii zenye asili na lugha moja pia. Ni makundi yanayofahamu

na kuzungumza lugha za jamii lakini kwa sababu mbalimbali za kijamii hupendelea kuzungumza zaidi Kiswahili kuliko lugha za jamii.

Baadhi ya sababu za kijamii zinazofanya makundi haya yatumie zaidi Kiswahili kuliko lugha za jamii ni hizi zifuatazo: Kwanza, Kiswahili ni lugha ya taifa inayowaunganisha watu wa makabila mbalimbali. Pili, kwa kuzungumza Kiswahili vizuri, mtu anaweza kupata kazi nzuri; Tatu, lugha ya Kiswahili inatumiwa na viongozi wa juu serikalini, kwa hiyo ina hadhi ya juu kuliko lugha za jamii; Nne, Kiswahili ni lugha inayotumika kujenga umoja wa kitaifa; Tano, Kiswahili ni lugha ya kimataifa na ni lugha muhimu barani Afrika; na sita kwa kuifahamu lugha ya Kiswahili vizuri, mtu yeyote anaweza kushiriki kikamilifu katika harakati za ujenzi wa nchi yake katika ngazi mbalimbali za uongozi.

Tunapenda tuisitize hapa kwamba kwa kuhimiza matumizi ya lugha za jamii vijijini, makundi yanayopendelea kutumia Kiswahili zaidi hayataathirika kwa namna moja au nyingine. Makundi haya bado yataendelea kutumia Kiswahili na kunufaika kutokana na umuhimu wa Kiswahili. Tunachosisitiza hapa ni kuyataka makundi haya (vijana, wasomi, wafanyakazi na wafanyabiashara) kujenga mazoea ya kutumia lugha zote mbili kikamilifu yaani Kiswahili na lugha za jamii. Mathalani, katika mazingira ya vijijini ambako watu wote ni wa asili na lugha moja, watu kama hao inafaa wahamasishwe kutumia lugha zao hata katika mazingira yaliyo rasmi kwa mfano: katika mahakama za mwanzo, hospitalini, kazini, kanisani, msikitini na kwenye mikutano mbalimbali ya hadhara. Kwa kutumia lugha za jamii miongoni mwa watu wa lugha moja, hakuna atakayejiona kuwa kabaguliwa kinyume na mazingira ya mijini.

Kuhamasisha matumizi ya lugha za jamii kwa njia hii kuna faida nyingi lakini sababu mbili ni za muhimu: Kwanza, kunatoa haki kwa lugha za jamii kutumika kama wazungumzaji wa lugha hizo wapendavyo. Pili, lugha za jamii zitakua kwa sababu wazungumzaji wa lugha hizi watapaswa kutafuta istilahi zinazostahili kutumika katika maeneo mapya ya matumizi. Istilahi za lugha za jamii zilizotaka kusahaulika au kupotea kutokana na kutotumiwa mara kwa mara, sasa zitatafutwa na kutumika.

Njia nyingine ya kuhimiza matumizi ya lugha za jamii vijijini ni kuanzisha vikundi vya umoja wa wakereketwa wa lugha za jamii. Umoja kama huu utakuwa na nguvu zaidi ikiwa utajumuisha makundi mengine ya kijamii kama: vijana, wazee, wasomi, wafanyabiashara, wafanyakazi na wanasiasa. Ni muhimu kwa makundi haya kushirikiana kwa sababu kila kundi litahamasisha kundi lake na kwa njia hii kutakuwa na kukamilishana. Ni rahisi kwa vijana kuwahamasisha vijana wenzao wapende kutumia lugha za jamii kuliko wazee kuwahamasisha vijana kwa lengo hilo hilo. Kuanzishwa kwa vikundi hivi vya umoja vya kuhimiza matumizi ya lugha za jamii huko vijijini siyo tu kutakuza lugha bali pia kutainua hadhi ya lugha hizi za jamii hapa nchini.

3.2 SERA YA LUGHA KUTAZAMWA UPYA

Kama tulivyosema katika 2.1.2, sera ya lugha ya Tanzania inachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha maendeleo ya lugha za jamii. Ili lugha za jamii ziweze kuimarika na kupata hadhi zinazostahili, sera ya lugha ya Tanzania haina budi kufanyiwa marekebisho ili iweze kutamka wazi dhima ya lugha hizi na jinsi lugha hizo zitakavyoendelezwa. Sera ya lugha inapaswa kutaja siyo tu vyombo vitakavyohusika katika kukuza na kuendeleza lugha hizi bali pia ihakikishe kwamba vyombo hivyo vinawezeshwa ili viweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Sera ya lugha ya Guinea ni miongoni mwa sera chache sana barani Afrika ambayo inakazia umuhimu wa kukuza lugha za jamii kwa ajili ya matumizi mapana ya kijamii. Kati ya lugha za jamii 20 za Guinea, lugha za jamii 8 zimeendelezwa na kufikia hadhi ya kuwa lugha za taifa. Lugha hizi ni: *Ful* (Peul, Fulani); *Manding* (Malinke, Mandinka); *Susu*; *Kisi*; *Kpelle* (Guerze); *Loma* (Toma); *Basari*; na *Koniagi* (Heine 1992: 31). Kuendelezwa kwa lugha hizi hadi kufikia hadhi ya kuwa lugha za taifa kunatokana na sera nzuri ya kuzithamini lugha hizi za jamii. Watunga sera nchini Guinea walichagua kwa makusudi mkabala wa kukuza lugha za ndani (zaidi ya moja) ili ziendelezwe sambamba na lugha ya kimataifa ya kutoka nje. Mpango huu wa sera ni mzuri kwa sababu lugha zote hupewa nafasi sawa ya kuendelezwa. Wakati lugha nane za jamii zinatumiwa kikamilifu kwa mawasiliano ya kitaifa, lugha ya Kifaransa nchini Guinea hutumiwa kwa mawasiliano ya kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wa Tanzania, kushuka hadhi kwa lugha za jamii kunatokana na sera ya lugha kufuata mkabala wa kuendeleza lugha moja ya ndani (Kiswahili) sambamba na lugha ya kigeni (Kiingereza) kwa mawasiliano ya kitaifa na kimataifa. Kwa mujibu wa sera ya lugha iliyopo ni vigumu sana kuinua hadhi ya lugha za jamii hapa nchini. Sera ya lugha ya Tanzania inahitaji kufanyiwa marekebisho ya msingi ikiwa tunataka kuinua hadhi ya lugha za jamii. Kwanza, sera ya lugha inatakiwa ifuate mkabala wa kukuza lugha kadhaa za ndani kwa mujibu wa vigezo vitakavyoonekana kufaa. Mathalani, sera ya lugha inaweza kuanza kuendeleza lugha zenye watumiaji wengi na kuishia kwa lugha zenye watumiaji wachache. Ieleweke hapa kwamba huu ni mpango wa muda mrefu na sio wa muda mfupi. Njia nyingine ni ile ya kuendeleza lugha za jamii kikanda kwa kufuata wazungumzaji ili kila kanda iteue lugha moja ya kuendelezwa. Mpango huu unatekelezeka ikiwa sera ya lugha itabadilika na kutamka hivyo.

Mbali na marekebisho ya msingi ya hapo juu, sera ya lugha haina budi kutamka wazi dhima ya kila lugha zinazotumiwa hapa nchini ili lugha hizo ziweze kuendelezwa kulingana na mahitaji ya jamii. Kwa mfano, nini dhima ya lugha ya Kiingereza hapa nchini? Tunajua Kiingereza ni lugha ya kimataifa inayotumiwa katika mawasiliano ya elimu ya juu, mahakama za juu, diplomasia, biashara na katika maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kisasa. Je, ni kwa kiasi gani lugha ya Kiingereza inatumika kiamilifu katika dhima yake hii? Ni wazungumzaji wangapi hapa nchini wanaomudu kuitumia lugha hii ya

Kiingereza kikamilifu katika maeneo ya matumizi yaliyotajwa hapo juu? Je, sera ya lugha inasema nini kuhusu wananchi wasio na umilisi wa kutumia Kiingereza ili nao waweze kunufaika sawa na wenzao? Ama kwa hakika, tunachojaribu kusisitiza hapa ni kuwataka watunga sera wapange upya dhima ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za jamii ili kuhakikisha kwamba dhima hizi mpya zinalingana na hali halisi ya watumiaji wa lugha wa hapa nchini.

3.3 KUHIMIZA MATUMIZI YA LUGHA ZA JAMII KATIKA VYOMBO VYA HABARI

Lugha yoyote huenea na kupata umaarufu ikiwa lugha hiyo inatumiwa sana katika vyombo vya habari kama vile katika redio, luninga na magazeti. Kuenea kwa lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na Kati na kwingineko ambako Kiswahili kinazungumzwa kumetokana na mchango mkubwa wa vyombo hivi vya habari. Ni kutokana na ukweli huu kwamba ikiwa tunataka kuinua hadhi ya lugha za jamii hatuna budi kwanza kujenga hoja ya kuwashawishi wamiliki wa vyombo vya habari watumie lugha za jamii katika vyombo vyao. Tunasisitiza umuhimu wa kujenga hoja kwa sababu tayari kumejengeka dhana miongoni mwa wananchi wa Tanzania kwamba kuhimiza matumizi ya lugha za jamii hapa nchini kutachochea ukabila na kuhatarisha umoja wa kitaifa uliojengeka kwa muda mrefu.

Tunapenda kusisitiza hapa kwamba umoja wa kitaifa hauna uhusiano wa moja kwa moja na nchi kutumia lugha moja. Umoja wa kitaifa unaweza kujengwa na kudumishwa hata katika nchi yenye lugha nyingi, mfano ni Tanzania. Kinachotakiwa katika kudumisha umoja wa kitaifa ni kwa viongozi husika kutawala na kutumia raslimali za nchi hiyo kwa misingi ya haki na kwa faida ya jamii kwa ujumla. Hata nchi yenye lugha moja inaweza kushindwa kujenga umoja wa kitaifa ulio imara ikiwa haki haitatawala. Nchi kama: Somali (Kisomali) na Ethiopia (Amharic), kila moja ina lugha yake kuu ya mawasiliano lakini nchi hizo zimeshindwa kujenga umoja wa kitaifa ulio imara.

Hata hivyo, uamuzi wa kutumia lugha za jamii katika vyombo vya habari hautawaliwi na wamiliki wa vyombo vya habari peke yao bali pia unatawaliwa na serikali kupitia katika sera yake ya lugha. Sera ya lugha ikiruhusu matumizi ya lugha za jamii katika vyombo vya habari, kazi ya wamiliki wa vyombo hivyo itakuwa ni kupanga idadi ya saa zitakazotumika kurusha matangazo ya vipindi vya lugha za jamii. Kwa mfano, redio nyingi duniani zinatangaza habari mbalimbali na vipindi maalum kwa lugha ya Kiswahili kwa saa zilizokubalika. Redio hizo ni kama: Beijing, BBC, Washington DC, Redio R.S.A., Redio Burundi n.k. (Dadi 1995). Hali kadhalika, Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ikiamua kutangaza baadhi ya vipindi vyake kwa lugha za jamii, lugha hizo siyo tu zitakua na kuenea bali pia zitaimarika na kudumu.

Tunahamasisha vyombo vya habari vitumie lugha za jamii kwa sababu muhimu zifuatazo: Kwanza, vyombo vya habari husaidia sana kukuza msamiati

wa lugha. Msamiati mpya husambaa kwa haraka sana kwa watumiaji na kwa njia hii, misamiati kama hiyo huzoeleka. Pili, vyombo vya habari husaidia kuhifadhi data za lugha. Watafiti hupata data za lugha za jamii kwa urahisi kutoka kwenye magazeti, kanda zilizorekodiwa na kwenye luninga. Tatu, vyombo vya habari pia husaidia kudumisha utamaduni wa jamii zinazohusika. Kwa njia hii, utamaduni wa taifa huimarika kwa sababu unakuwa umejengeka katika tamaduni zilizo hai. Sababu nyingine ni kwamba vyombo vya habari husaidia kueneza lugha ndani na nje ya mipaka ya nchi. Vyombo vya habari vikiamua kutumia lugha za jamii, lugha hizi siyo tu zitaenea mbali bali pia zitatumika na watu wengine wasio wa lugha hizo kwa madhumuni ya kutaka kuwasiliana na wazungumzaji wa lugha hizo za jamii.

3.4 LUGHA ZA JAMII KUPEWA HAKI YA KUTUMIKA KISHERIA

Mbinu ya uhakika ya kuzifanya lugha za jamii zitumike kikamilifu katika mawasiliano ya jamii ni kwa lugha hizo kupewa haki ya kutumika kisheria. Sheria ikiruhusu matumizi ya lugha za jamii hapa nchini, itasaidia sana siyo tu kuzilinda lugha hizi bali pia kuzipa hadhi ya kutumika katika nyanja mbalimbali za kijamii. Mafanikio ya lugha ya Kifaransa ya kutumika kiamilifu katika shughuli zote rasmi za serikali, elimu, mahakama, biashara na katika sayansi na tekinolojia katika jimbo la Quebec nchini Canada yametokana na kupitishwa sheria inayoruhusu matumizi ya lugha hiyo (Josiane F. Hamers and Kirsten M. Hummel 1994). Sheria hiyo ilipitishwa kwa lengo la kulinda matumizi ya lugha ya Kifaransa ambayo imezungukwa na wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiingereza.

Tunapenda kuisitiza hapa kwamba ikiwa sheria hazitatungwa kulinda haki za lugha za jamii kutumika katika maeneo ya matumizi yaliyoteuliwa, uhai wa lugha hizi utakuwa mashakani. Tunasema hivi kwa sababu watumiaji wa lugha hizi watasita kutumia lugha za jamii hadharani kwa kufikiri kwamba wanafanya makosa ya kuchochea ukabila. Kwa maoni yetu, huku kukosekana kwa sheria zinazolinda haki za lugha hapa nchini, kumerudisha nyuma siyo tu kasi ya maendeleo ya lugha za jamii bali pia kasi ya maendeleo ya Kiswahili. Pamoja na ukweli kwamba Kiswahili ni lugha ya Kimataifa, iliyosanifiwa, yenye istilahi za kutosha katika nyanja mbalimbali, bado hadi leo Kiswahili hakitumiki kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na elimu ya juu. Moja ya sababu ya msingi inayochelewesha utekelezaji huu usifanyike, inatokana na ukweli kwamba Kiswahili siyo lugha rasmi kisheria. Kama ingekuwa imetamkwa kisheria kwamba Kiswahili ni lugha rasmi ya taifa, serikali ingekuwa imeshaamua kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika elimu ya juu. Ingefanya hivyo kwa kubanwa na sheria. Ni kwa mantiki hii, tunasema kwamba hata lugha za jamii zina haki ya kulindwa kisheria ikiwa tunataka lugha hizi zisitoweke hapa nchini.

4. HITIMISHO

Katika majadiliano yetu tumeona kwamba hadhi ya lugha za jamii hapa nchini imeshuka sana hasa ukilinganisha na lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Kigezo kilichotumika kupima hadhi za lugha mbalimbali ni kile kinachohusisha lugha moja na lugha nyingine za nchi zilizoendelea kiuchumi. Lugha zinazoelezea maendeleo ya juu ya kiuchumi hupewa hadhi ya juu kuliko zile zinazoelezea maendeleo ya kiuchumi ya nchi zinazoendelea.

Katika uchunguzi wetu tumebaini kwamba kuna sababu kuu mbili zinazochangia kushuka kwa hadhi ya lugha za jamii hapa nchini. Sababu ya kwanza inatokana na lugha za jamii kutotumika rasmi katika mawasiliano ya maendeleo ya jamii. Hii ina maana kwamba lugha hizi hazikidhi mahitaji ya mabadiliko na maendeleo ya kiuchumi ya jamii. Sababu ya pili inatokana na udhaifu wa sera ya lugha. Kama sera ya lugha haitamki wazi kuziendeleza lugha hizi za jamii, hadhi ya lugha hizi zitaendelea kushuka chini zaidi. Ili kuinua hadhi ya lugha hizi za jamii, makala haya yanapendekeza mbinu zifuatazo zitumike. Kwanza, wazungumzaji wa lugha hizi wahimizwe kutumia lugha zao za jamii; Pili, sera ya lugha ya Tanzania ifanyiwe marekebisho ya msingi ili lugha za jamii ziweze kuendelezwa; Tatu, vyombo vya habari vihimizwe kutumia lugha za jamii katika vyombo vyao ili kueneza na kudumisha lugha hizi; na mwisho, lugha za jamii hazina budi kupewa haki ya kutumika kisheria hapa nchini ili ziweze kukuzwa na kuendelezwa kama zilivyo lugha nyingine.

MAREJEO

Abdulaziz-Mkilifi, M. H. 1972.

Triglossia and Swahili – English Bilingualism in Tanzania. Language in Society, 1(1): 197–213.

Appel, R. and Muysken, P. 1987.

Language Contact and Bilingualism. London: Edward Arnold.

Batibo, H. M. 1992.

The Fate of Ethnic Languages in Tanzania. In: M. Brenzinger (ed.), *Language Death: Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa*, p. 85–95. Berlin: Mouton.

Blommaert, J. 1990.

Standardization and Diversification in Kiswahili: A Note on Language Attitude. Kiswahili, 57: 22–32.

Brauner, S. K. L. and Kapinga, C. 1978.

Kiswahili and Local Languages in Tanzania. Kiswahili, 48(2): 48–72.

Dadi, K. S. 1995.

Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Msamiati. Katika: S. A. K. Mlacha (Mhariri), *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.

- Hamers, J. F. and Hummel, K. M. 1994.
The Francophones of Quebec: Language Policies and Language Use. Journal of Sociology of Language, 105/106: 127 – 152.
- Heine, B. 1992.
Language Policies in Africa. In: R. Herbert (ed.), *Language and Society in Africa. The Theory and Practice of Sociolinguistics*, pp. 23–35. Cape Town: Witwatersrand University Press.
- Kaplan, R. B. and Baldauf, R. B. 1997.
Language Planning: From Practice to Theory. Clevedon: Multilingual Matters.
- Kihore, Y. M. 1983.
Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika. Mulika, 15: 32–39.
- Mekacha, R. D. K. 1993.
The Sociolinguistic impact of Kiswahili on Ethnic Languages in Tanzania: A Case Study of Ekinata. Bayreuth: Bayreuth African Studies Series.
- 2000 *Ismujamii: Nadharia ya Muktadha wa Kiswahili*. Minoo City, Osaka. Osaka University of Foreign Studies.
- Milroy, J. 1984.
The History of English in the British Isles. In: P. Trudgill (ed.), *Language in the British Isles*. London: Cambridge University Press.
- Msanjila, Y. P. 1999.
The Use of Kiswahili in Rural Areas and its Implications for the Future of Ethnic Languages in Tanzania. Ph.D. Thesis, unpublished. University of Dar es Salaam.
- Whiteley, W. 1969.
Swahili: The Rise of a National Language. London: Methuen.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni. 1997.
Sera ya Utamaduni, Dar es Salaam.

About the author: Dr. Yohana P. Msanjila is a Senior Research Fellow in the Institute of Kiswahili Research at the University of Dar es Salaam. He has published a lot in the area of macro-sociolinguistics focusing on language policies, language in education and on the future of ethnic community languages in Tanzania.